

## Athari ya Washairi Wakongwe Juu ya Washairi wa Kisasa: Mfano wa Muyaka Bin Haji na Ahmad Nassir

G.K. King'ei

Idara ya Kiswahili na Lugh za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta

### Ikisiri

Kwa kutumia vichwa vya mashairi, umbo na mtindo, msamiati na maudhui, makala hii inavitambulisha baadhi ya vipengele vya usanifu vinavyopatikana katika ushairi wa Muyaka wa Muhaji na jinsi ambavyo vipengele hivyo vimeathiri, kila kimoja kwa kiasi chake, ushairi wa Ahmad Nassir katika diwani ya *Malenga wa Mvita*. Makala inatumia tungo za Muyaka zilizochambuliwa na Mohamed Hassan Abdulaziz na kuchapishwa mwaka wa 1979. Humu mnaonyesha kiwango cha athari za ushairi wa Muyaka na kuthibitisha jinsi mvuto mkubwa na usanifu wa tungo za Muyaka uliyowapendeza washairi wa karne ya ishirini kama Ahmad Nassir.

### 1:0 Utangulizi.

Bila ya shaka yoyote, Muyaka Bin Haji (1776-1840) ni mionganoni mwa waasisi wa ushairi wa Kiswahili, hasa utanzu wa bahari za “shairi”. Kulingana na Abdulaziz (1979:ix),

“Ingawa Muyaka alikuwa mshairi aliyetoka kisiwani Mombasa, usanifu wake juu ya umbo na mtindo wa mashairi umedumu hadi leo na umeathiri baadhi kubwa ya watanzi wa mashairi waliokuja baada yake”.

Yumkini baadhi ya washairi walioathiriwa sana na Muyaka ni pamoja na wale wa rika lake kama vile A.A. Nassir (1720-1840) aliyetunga *Takhmis ya Liyongo* na pia *Utenzi wa Liyongo*; mtunzi wa *Mwanakupona* na pia watuzi wengine wa wakati wake kama vile Songora Mkilifi, Jinga na wengineo (Abdulaziz 1979). Hata hivyo, ingawa usanifu wa washairi wengi wa kale umewahi kuchambuliwa kwa undani na wasomi wa Kimagharibi kama vile Allen, Harries, Parker, Hichens, Taylor, Knappert and Whiteley mionganoni mwa wengine, athari ya Muyaka juu ya washairi wa hapo baadaye kama vile Shaaban Robert, Mathias Mnyampala, K.A. Abedi na K.H.A. Akilimali bado haujafafanuliwa vilivyo. Uchambuzi wa ushairi wa kisasa hauwezi kukamilika bila ya kukihakiki kipengele hiki na kukadiria kiasi cha athari zake kutokana na washairi wakongwe kama Muyaka.

Makala hii fupi itajaribu kutoa mifano kudhihirisha madai ya Abdulaziz kwamba Muyaka aliweza kuathiri ushairi wa kisasa (baada ya karne ya 19) katika viwango tofauti. Mfano wa mshairi aliyeteuliwa kuwakilisha kipindi cha kisasa cha ushairi na ambaye anadhihirisha kiwango kikubwa cha athari kutokana na Muyaka ni Ahmad Nassir, ambaye kama Muyaka, ni mzaliwa wa kisiwani Mombasa. Mshairi huyu ni mojawapo wa wasanii wa karne iliyopita ya 20 ambao kazi zao zimepata sifa za kimataifa. Mionganoni mwa machapisho yao yanayojudikana zaidi ni *Malenga wa Mvita* (1971) na *Taa ya Umalenga* (1977). Makala hii itatumia mifano ya mashari kutoka katika diwani maarufu ya *Malenga wa Mvita*.

### 1:1 Mtazamo wa Kinadharia

Kwa nini Nassir aliathiriwa na ushairi wa Muyaka aliyetunga karibu karne tatu kabla yake? Je, inawezekana kwamba kati ya mwaka wa 1840 na miaka ya 1970 hapakutokea washairi wengine wa Kimvita au Lamu ambao kazi zao zilikuwa na mvuto kama vile ile ya Muyaka? Iwapo ni kweli Nassir aliathiriwa sana na kazi ya Muyaka, kwa nini hakuiga ushairi wa Muyaka wa maudhui ya vita na kisasa? Je yawezekana kwamba katika kipindi hicho cha historia ya ushairi

wa Kiswahili katika kisiwa cha Mombasa na mwambao wa pwani ya Kenya kulikuwa na mazingira sawa ambayo yaliwaathiri washairi Muyaka na Nassir kwa njia sawa?

Ujumi wa kipindi fulani cha maendeleo ya sanaa kama vile ushairi haupaswi kuchukuliwa kuwa kitengo maalum cha usanifu bali unapaswa kuhesabiwa kama kielelezo cha amali na mitazamo ya jamii nzima (Eagleton, 1983:21). Hii ina maana kuwa pengine ujumi wa kipindi cha ushairi kati ya Muyaka na Nassir uliwaathiri wote kwa njia sawa ; au huenda Nassir alifuata hatua za Muyaka kutokana na mvuto wa kazi zake Muyaka aliyemtangulia.

Baadhi ya vipengele vya usanifu wa kishairi vinavyoweza kudhihirisha athari za Muyaka juu ya A. Nassir, kama mwakilishi wa washairi wa karne ya 21, ni kama vile:

- vichwa vya mashairi
- uteuzi wa maneno (msamati)
- miundo ya kishairi (mitindo)
- maudhui

## 2:1 Vichwa vya Mashairi.

Baadhi ya vichwa au anwani za mashairi yaliyosifika sana ya Muyaka bin Haji vimetumiwa kwa mapana na jumuiya ya washairi wa kisasa wala sio tu Ahmad Nassir. Mfano mmoja wa kichwa kama hicho ni “**Oa**” Katika shairi hili, Muyaka alikusudia kufafanua kwa namna ya ukinzani maana tatu tofauti za neno “oa”. Maana ya kwanza ni **kufunga ndoa**. Kwa mfano:

“Oa mwanamke tama, mtukufu wa stawa”

Au: “Oa uole wapambe, wako ulopambiwa” (Abdulaziz:182).

Maana ya pili ni **angalia** au **tazama**. Kwa mfano: “Oa mato maolezi, na mboni ukikondoa”.

Maana ya tatu ni “oga” au “ogelea ”. Mathalani: “Oa maji maundazi, meupe kama maziwa”.

Kichwa hiki “Oa” kimetumiwa na washairi wengi wa kisasa, kama vile Akilimali alipotunga shairi “Oa” (1952-53) kwa maana ya “funga ndoa”. Ubeti wa kwanza unasema:

Oa mwana maridhawa, oa mrembo jamali.  
Oa mwana mlelewa mwenye utu mwenye hali,  
Oa sioe beluwa, sio mke fedhuli  
Oa mwana kwetu oa, oa mrembo jamali. (52)

Mshairi mwingine aliyetumia kichwa “Oa” kwa maana ya “funga ndoa” ni K.A. Abedi (1954). Ikumbukwe kuwa mtindo huu wa kubuni shairi fulani upya kimaudhui umewahi kutumika katika miaka ya hivi karibuni ambapo washairi kadha walilirudia na kulisarifu upya shairi maarufu la Abdilatif Abdalla liitwalo, “Usiniwe”. Baadhi walilitunga na kuliita “Nimekuua”, “Nitakuua”, “Nishakuua” na kadhalika (Abdalla 1976: )

Mshairi Ahmad Nassir alikichukua kichwa hiki na kukifafanua zaidi kwa kuzidisha au kurefusha wingi wa sifa za mke afaaye kuolewa. Kama Ilivyokuwa kwa Muyaka, Nassir alilenga kutoa ushauri au nasaha kwa yeoyote aliyetaka kufunga ndoa. Kinyume na Muyaka aliyetunga beti 6 tu tena zenye maana tatu tofauti za neno “oa”, ( Kimvita: “owa”), Nassir alitunga shairi la beti 12 akitumia maana moja tu ya ndoa na mke anayestahiki kuolewa. Ubeti wa mwanzo unasema:

Owa sandame hadaa, moyo ukahadaiwa  
Owa anaye kufaa, mke mwenye kusifiwa  
Upate upate kuzaa, kama ulivyozaaliwa

Owa ukijaliwa, upendane na mkeyo” (158).

A. Nassir aliiga mtindo wa Muyaka wa kutunga shairi linalotumia neno moja na kulipa maana tofauti katika kila mshororo. Vichwa vyatashairi ya Muyaka yenye muundo na mtindo huu ni : **Oa** (182-183); **Panda** (190); **Jinga** (186); **Sichi** (184); **Kimya** (194); **Mahaba** (184), na **Aha** (188).

Katika tungo za Nassir zilizomo katika *Malenga wa Mvita (MWM)*, mifano ya mashairi yenye kutumia neno moja ni kama vile: Panda (76), Twaa, (78), Tunga (80) na Kimya (82). Tukichunguza shairi “Panda” na “Kimya” tutagundua ukuruba mkubwa baina ya mtindo na maudhui ya Muyaka na yale ya Nassir. Wote wawili wana nia ya kuelema maana tofauti na wote wana mtindo wa kuanzisha kila mshororo kwa neno lilo hilo “panda”. Beti za zao za kwanza zinasema:

Panda, panda la mnazi, l’anzalo kupapatuka  
Panda juu ya malazi, moyo wako weshe ngowa  
Panda mti wa mapenzi, uwepushie na juwa  
Panda ni wako uluwa. Panda darajani, panda. (Muyaka: 190)

Panda mwana mpandifu, nikueleze shairi  
Panda lenye ashirafu, jambo jema la fahari  
Panda zisiche ulufu, Hata zikawa kururi  
Panda usitaakhari, ingawa pindi mwakani” (Nassir: 76)

Muyaka ametunga kuonyesha maana za neno **panda** kama vile: panda la mnazi, yaani matawi yenye kuachana na kufanya panda; kwea juu; panda mbegu na zidi katika daraja au heshima. Kwa upande wake, Nassir amefafanua maana tatu za neno hilo nazo ni: kwea juu; tenda jambo jema na pata cheo cha juu (daraja). Hata hivyo tukilisoma kila shairi kwa ukamilifu, tutagundua kiwango kikubwa cha kufanana kimaana kati ya mashairi haya. Kwa muhtasari washairi wote wawili wanahimiza watoto wao wawe na tabia njema ili waweze kuwa watu wenye utu maishani.

Hali kadhalika, katika shairi lao la “Kimya”, wote wawili wanajaribu kuasa watu wawe na kiasi katika kusema na kutenda wala wasiwadharau wale walionyamza na walio wapole kwani upole na unyamavu sio dalili ya ujinga ua woga bali ni ishara ya wekevu na umaizi wa mambo. Inafaa kuwa na tahadhari na kufikiri kabla ya kutenda au kujisemea ovyo. Hebu tulinganishe ufananifu wa maudhui katika beti hizi mbili:

Kimya vuani maozi, vuani mato muole  
Kimya kitaangusha mwanzi, mwendako msikujule  
Kimya chatunda p’umuzi, kiumbizi kiumbile  
Kimya kina mambo mbele, tahadharini na kimya. (Muyaka :194)

Kimya kizingatieni, mukome na kukisema  
Kimya kisitukakeni, na vigumba kkukifuma  
Kimya chaja bwaga zani, wa mbele awe wa nyuma  
Kimya kiwapo si chema, na maneno hayafai. (Nassir:83)

## 2:2 Msamiati

Hapana shaka kwamba Nassir kama vile Muyaka kabla yake, alitumia kwa mapana na marefu msamiati na matamshi yanayotokana na lahaja yake ya Kimvita. Lahaja hii ilipewa umaarufu mkubwa na ushairi wa Muyaka wa Muhaji kulingana na uchambuzi wa tungo zake katika

Abdulaziz (1979). Mifano ya matamshi ya Kimvita yakilinganishwa na yale ya Kiswahili sanifu ni kama yafuatayo:

<b>Kimvita</b>	<b>Sanifu</b>
N'nayo	ninayo
Naata	naacha
Kaani	kaeni
Hishima kupaana	heshma kupeana
Muchamba	mkiamba
Kuteza	kucheza
Vutani	vuteni
Chaja zua	kitakuja kuzua
Kinyemele (kikae)	kimenyamaza
Mejieka	(ni) mejiweka
Mitima (kikae)	mioyo
Uyuwao	ujuaye
Ndiya	njia
Sipije mbizi	usipige mbizi
Fumbua mato	fumbua macho
Mambo mapendezi	mambo ya kupendenza
Yampayo mtu kukuwa	yamwezeshayo
Ukomele kina	mtu kukua
Kiteza nami	ufikie kina
Yana	akicheza na mimi
Nima	jana
	nyuma

Baadhi ya msamiati walotumia washairi hawa ni asili ya Kiarabu na wanaandika kwa matamshi hayo hayo ya Kiarabu ambayo ni tofauti kidogo na matamshi ya Kiswahili sanifu. Mifano:

<b>Msamiati wa Kiarabu</b>	<b>Sanifu</b>
Ashirafu	utukufu
Ulufu	maelfu
Khofu	hofu
Kheri	heri
Khatuwa	hatua
Kulla	kila

Pia Nassir ametumia msamiati wa **kizamani** yaani **kikae** (pengine huitwa lahaja ya Kingozi) uanofanana na ule alioutumia Muyaka zaidi ya karne tatu kabla. Mifano:

<b>Kikae</b>	<b>Sanifu</b>
Ndimi mwavigambo	Ni mimi mwenye kujigamba
Mfungata sombo	mwenye kujifunga kiunoni
Narudi kuwana	naja kupigana
Bangu	vita
Mbonezani	nionyesheni
Likikwela	likikwea
Ninyemele	nimenyamaza
Nambayo	nisemayo
Ungoi	uhodari
Vumbile silichi	vumbi lake siliogopi
Uyatenzileyo	uliyoyafanya

Ushishiyeo	uliyoyashikilia
Alileni?	Alikula nini?
Kukowa	kuogelea au kuoga

### 2:3 Umbo na Mtindo

Pana ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa Nassir alifuata sana mitindo ya ushairi aliyoivyaza Muyaka zaidi ya karne mbili kabla yake. Baadhi ya mtindo ni ule utungo wa “nudhuma” ambapo mshairi hutumia neno lile lile kuanzishia kila mshororo katika shairi zima. Athari za Muyaka juu ya Nassir katika kipengele hiki ni dhahiri ukilinganisha mtindo na uteuzi wa maneno na pia maudhui katika beti hizi:

Owa ndiwe muolezi, uzoweleo kuowa  
 Owa sifumbe maozi, maninga uchiyavuwa  
 Owa uzaze uzazi, kama ulivyo zaliwa  
 Owa sizi ndizi ndowa, asokuowa ni yupi? (Muyaka)

Owa sandame hadaa, moyo ukahadaiwa  
 Owa anayekufaa, mke mwene kusifiwa  
 Owa upate kuzaa, kama ulivyo zaliwa  
 Owa ukijaliwa, mupandane na mkeyo. (Nassir)

Kama Muyaka, Nassir ametumia ‘tarbia ya aina ya nudhuma inayoanza kwa “owa” na ametumia pia mazani 8/8 kwa kila mshororo huku pia akiazima kina cha mwisho mwa mshororo yaani “wa” kutoka kwa Muyaka. Nassir, kama Muyaka ameunga kila mshororo wake kwa kutia kina cha ndani katika mizani ya 8. Mwisho pia tunamwona Nassir akimwiga Muyaka katika kutia kipokeo au mkarara katika msitari wa mwisho katika kila ubeti kwa shairi lote.

Ingawa Nassir ametunga mashairi machache ya tathlitha (mistari mitatu) kama vile katika ngonjera yake maarufu, “Mkufuu na Mwanafuu” (65), “Maskini” (106), “Moyo” (109) na “Mja” (117), takribani asilimia tisini ya tungo zake zote katika diwani hii ni yenye muundo wa tarbia kama ule wa Muyaka. Baadhi kubwa ya tungo za Nassir za tarbia zina muundo sawa na wa Muyaka, yaani:

A	b
A	b
A	b
B	x

Kina cha sita hupinduliwa na kuwa kina cha saba ilhali, kina cha mwisho au cha kituo huwa ni tofauti na vina vingine vya ubeti na hurudia katika shairi zima. Mifano:

Kongowea yaugua, kwa kite na uuguzi  
 Kwa mabo kuyageua, kugeua mageuzi  
 Rabi, Ngwaipa afua, na kuiifu si kazi  
 Kutanani wamaizi, shauri jema mtende. (Muayaka: 202)

Nali meketi makini, ukanjia na vita  
 Nami hangia vitani, usiweze kuviteta  
 Kulla mngiya mvuani, hana budi kutota  
 Sizidishile matata, kapumzike utuwe. (Nassir:41).

Muyaka alizua mtindo maarufu wa kutumia “risala, mjumbe au mtume” asiyefahamika ili kupeleka tarifa au ujumbe wa shairi lake. Mtindo huu wa kimazungumzo ulitokea kuwa maarufu sana katika karne ya 20 hasa kaatika tungo za Shaaban Robert. Pana ushahidi kwamba Nassir aliaithirika na mtindo huu wa Muyaka katika tungo zake katika diwani ya *Malenga wa Mvita*. Inaelekea kuwa Muyaka aliupata mtindo huu wa kimazungumzo na mhusika “bubu” kutohana na

mbinu za nyimbo za kimapokezi za Waswahili zilizokuwepo hata kabla ya yeze kuanza kutunga. Katika mfano ufuatao wa wimbo wa vugo, mwimbaji anasema na mhusika “bubu” katika mstari wa kwanza:

P’ani kiwanda niteze, polepole mtu mweni (Muyaka:56)  
Risala wangu basiri, kambe nao washupavu (Muyaka:170)  
Karatasi ya Kishamu, fuitana na mzungu (Muyaka:178)  
Risala wangu basiri, leo napenda kutuma (Muyaka: 200)

Karatasi ya Turuki, njema usio shahiba  
Nakutuma kwa rafiki, kwa fundi wa Taliha  
Sipumbae kwa madhiki, lete neno la nasaha  
Mgosi hana fedheha, utangia makosani (Muyaka:210)

Kwa upande wa Nassir, tunapata matumizi ya mtume kama haya:

Mwendani enuwa kimo, msalimpoo sinikabe (Nassir: 40)  
Pani kalamu ya tungo, nitungamanishe vina (46)  
Kiswahili nakutuma, lugha njema ya maani (50)  
‘Pani nami karatasi, ya ngozi ilo adimu (55)  
Risala enuka hima, ‘sikae kataghafali (63)

Risala wa Ahmadi, mtungaji mashuhuri  
Nakutuma jitahidi, wenende pasi usiri  
Mwambie atabaradi, mwenzawa atafakuri  
Yangawa mangi mahari, na’fikiri gharama (69)  
Panda mwana mpandifu, nikueleze shairi (76)  
Risala mnena wazi, leo nataka kutuma (82).

Pia Muyaka na Nassir wametumia sana lugha yenye mafumbo ya kina kirefu kama beti hizi zinavyoonyesha. Katia ubeti huu, Muyaka anaajabia matamanio ya moyo wa binadamu na anajaribu kuonyesha kuwa baadhi ya tamaa za moyo wa mtu haziwezi kutimizika.

Moyo wanambia kwamba, jambo la mtu usambe  
Moyo wanambia omba, kitu cha mtu siombe  
Moyo wanambia ramba, tete ya moto sirambe  
Moyo watamani pembe! Ilo na ndovu kitwani (Muyaka:96).

Kwa upande wake, Nassir ametenga sehemu nzima ya mashairi ya kufumba ambapo anadhihirisha usanifu wake wa lugha ya kimafumbo kama mshairi. Katika mifano ifuatayo ya mashairi ya mafumbo, Nassir anafumbia mambo tofauti.

- Kitu gani duniani kisichoumbwa na M’ungu? (59)
- Nauliza Kiswahili, ni lugha ya watu gani? (63)
- Iwapo wamtambua, nambia ni ndege gani? (65)

## 2.4 Maudhui

Inaelekea athari ya Muyaka kwa Nassir haikukomea kwenye kiwango cha kuazima vichwa au anwani za mashairi ya Muyaka. Mtunzi huyu Nassir, alitenga sehemu nzima ya mashairi katika diwani yake ili kutoa fasili au ufanuzi wa maudhui ya baadhi ya tungo za Muyaka. Kulingana na utangulizi wa Shihabuddin Chiraghdi, mhariri wa diwani wa *Malenga wa Mvita*, Ahmad Nassir “... aliyasherehe mashairi ya Muyaka ili kudhihirisha ujuzi wake wa fani ya ushairi na hasa pia kuwaani wale walioitingwa na ugumu wa lugha ya kizamani ya Muyaka.”

Kwa kumuiga Muyaka, Nassir ametunga mashairi mengi ya kuonesha umahiri wake kama mshairi, yaani kujigamba kishairi kama alivyofanya Muyaka. Hapa tuna mifano ya tungo kama hizo za majigambo yake Muyaka na Nassir.

**Muyaka:**

- (a) Ndimi Muinda (176)
- (b) Kiwiji simba wa maji
- (c) Silichi

**Nassir**

- (a) Malenga (28)
- (b) Wawapi wajigambao? (30)
- (c) Sinitisheni (36)

Kwa hakika, mbali na kwamba Muyaka alitunga mashairi mengi sana kuhusu hali ya vita kati ya miji ya Mombasa, Pate, Lamu na Unguja, maudhui yake yote mengine yamerudiwa kwa kiasi fulani cha ubunifu na Nassir katika *Malenga wa Mvita*. Maudhui hayo ni kama vile:

- maisha ya kibinagsi,
- falsafa kuhusu maisha,
- mapenzi na uhusiano kati ya wake na waume,
- kujigamba kishairi, na
- mawaidha ya aina mbalimbali.

## 2.5 Hitimisho

Makala hii imejaribu kuvitambulisha baadhi ya vipengele vya usanifu vinavyopatikana katika ushairi wa Muyaka wa Muhaji na jinsi vipengele hivyo vilivyoathiri kwa njia fulani au moja kwa moja ushairi wa Ahmad Nassir katika diwani ya *Malenga wa Mvita*. Mifano ya tungo za Muyaka imetolewa katika uchambuzi wa kazi hizo uliofanywa na Mohamed Hassan Abdulaziz na kuchapishwa mwaka wa 1979.

Ili kuthibitisha kiwango cha athari za Muyaka juu ya Nassir, makala imetumia vipengele kama vile: vichwa vya mashairi, umbo na mtindo, msamiati na maudhui. Kiwango cha athari kilichodhahirishwa kinaonyesha mvuto mkubwa wa tungo za Muyaka na jinsi usanifu wake ulivyowapendeza washairi wa karne ya ishirini kama Ahmad Nassir.

Hata hivyo, kuna haja ya kuchunguza athari za ushairi mkongwe juu ya ushairi wa kisasa. Bila shaka washairi wa zama kama vile Liyongo, A.A. Nassir (1720-1840), Mwanakupona (1800-1860) na wengineo, wamekuwa na mchango mkubwa sana katika maendeleo ya ushairi wa kisasa.

## Marejeo

- Abdalla, A. (1976). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.
- Abedi, K. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Abdulaziz, M. (1979). *Muyaka: 19<sup>th</sup> Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Akilimali, K. (1969). *Diwani ya Akilimali*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Eagleton, T. (1983). *Literary Theory: An Introduction*. Oxford: Blackwell.
- Harries, L. (1962). *Swahili Poetry*. London: Oxford University Press.
- Hichens, W. (1939). *Al-Inkishafî*. London: Oxford University Press.
- Knappert, J. (1967). *Traditional Swahili Poetry*. Leiden: E.J. Brill.
- \_\_\_\_\_, (1971). *Four Centuries of Swahili Verse*. London: Heinemann.
- Mnyampala, M. (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Nabahany, A. (1972) Mhar. *Utenzi wa Mwanakupona na Utenzi wa Ngamia na Paa*. Nairobi: Heinemann.
- Nassir, A. (1971). *Malenga wa Mvita*. Nairobi: Oxford University Press.
- \_\_\_\_\_, (1975). *Taa ya Umalenga*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Nassir, S. (angalia Hichens hapo juu).
- Parker, L. (1969). "Musical Analysis of Two Swahili Meters", *J.I.R.R. Toleo* 37/2 (180-188).
- Taylor, W.E. (1964). *African Aphorisms*. London: S.P.C.K.
- Whiteley, W.H. (1955). *Journal of the East African Swahili Committee*. No.25.